



# ARUSHA MEAT COMPANY LTD

P. O. BOX 14167

ARUSHA

TANZANIA

E-mail: [arushameatcompany@yahoo.com](mailto:arushameatcompany@yahoo.com)

TEL: +255 272970304

Mob: +255734026767

**KUMB. NA. AMCO/STF/O10/44**

**DATE: 01/08/2023.**

## **TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI (RE-ADVERTISED POST).**

Arusha Meat Company Limited ni Kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria za Makampuni ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inajishughulisha na huduma ya uchinjaji wa ng'ombe, mbuzi na kondoo. Aidha Kampuni hii pia huchakata nyama kwa ajili ya kutengeneza bidhaa mbalimbali. Tangazo hili la ajira linarejea tangazo la awali la ajira lenye **Kumb.Na. AMCO/STF/O10/43** la tarehe **06 Julai, 2023** lililokuwa limetangazwa, sasa **limehuishwa** tena kwa ajili ya kuwapata waombaji wenye sifa stahiki kwa nafasi ya Mchakataji nyama (Meat-Processor). Hivyo waombaji wote wenye sifa, mnakaribishwa. Kwa wale waombaji ambao awali walishatuma maombi kwa nafasi hii hamtahitajika kuomba tena.

### **1.0 MCHAKATAJI NYAMA (MEAT-PROCESSOR) NAFASI TATU (3).**

#### **1.1 MAJUKUMU YATAKUWA KAMA IFUATAVYO:**

- i. Kutenganisha nyama na mifupa.
- ii. Kucharanga mifupa tayari kwa kuuzwa dukani, kutayarisha mikato ya nyama mfano Primecut, Back kwa mikato ya T-bone steak, shin kwa mikato ya ossobuco, sirloin, beef fillet pamoja na nyama za kutengeneza soseji.
- iii. Kufungasha bidhaa zote za nyama zilizochakatwa na kuzikabidhi kwa mtunza stoo kwa maandishi (parking ledger).
- iv. Kufanya usafi kwenye maeneo yote ya uzalishaji pamoja na mitambo yote yaani vitendea kazi.

- v. Kujaza taarifa kwenye vitabu vya uzalishaji (Production Ledger).
- vi. Kufanya jukumu jingine lolote atakalopangiwa na Mwajiri.

## **1.2 SIFA ZA MWOMBAJI.**

- i) Awe na Astashahada katika fani ya Sayansi ya chakula na uzalishaji, Cheti cha uchakataji nyama au sifa sawa na hizo kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali.
- ii) Mwenye uzoefu usiopungua mwaka mmoja (1) katika fani hiyo atapewa kipaumbele.
- iii) Awe na umri usiozidi miaka 45.

## **1.3 MSHAHARA:**

Kwa kuzingatia ngazi ya Mishahara ya Arusha Meat Co. Ltd yaani ngazi ya **AMC 2.**

## **MASHARTI YA JUMLA KWA NAFASI ZILIZOTANGAZWA.**

- i. Waombaji wawe raia wa Tanzania.
- ii. Waombaji waambatanishe vyeti vya kuzaliwa.
- iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu pamoja na barua iliyoandikwa kwa mkono na kusainiwa.
- iv. Anuani na namba ya simu ya mwombaji na picha moja "Passport size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.
- v. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, nakala za vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika vyeti vya kitaaluma (professional certificate) kutoka bodi husika na viwe "Certified".
- vi. "Testimonials" "provisional results" "statement of result" hati matokeo za kidato cha nne na sita **HAVITAKUBALIWA.**
- vii. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na mamlaka husika (TCU, NECTA, NACTE).
- viii. Mwombaji atajigharamia mwenyewe wakati wa usaili.

ix. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili

**HAYATAPOKELEWA.**

x. Ajira hii ni ya mkataba wa muda maalumu.

**NB:** Barua zote za maombi zitumwe kwa njia ya Posta kwa anuani ifuatayo:

MENEJA MKUU,

ARUSHA MEAT CO. LTD,

S.L.P 14167,

**ARUSHA-TANZANIA.**

**NB:** Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 14/08/2023. Aidha kwa waombaji wengine waliotuma maombi kupitia tangazo la awali kwa nafasi za Uchunaji (Skinners), Mtaalamu wa TEHAMA (IT-Technician) na Mhudumu wa Ofisi (Office Attendant), usaili utaendelea kwa tarehe itakayopangwa kwa wale wenye sifa zinazohitajika wataitwa kwenye usahili huo.

Imetolewa na: -

STEPHEN L. SULTAN

**MENEJA MKUU**

ARUSHA MEAT CO. LTD

**Nakala:**

➤ Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi (AMCL),

S.L.P 14167,

**ARUSHA.**

➤ Mbao za matangazo.

➤ Tovuti ya Kampuni.